

0001 kati ya 0010

SEHEMU A: (Alama 20)**UFAHAMU**

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Mzee Nyange ana upungufu wa meno kadhaa kinywani mwake, hivyo watu walimpachika jina la kibogoyo. Mwanzoni alichukia sana kuitwa jina hilo, lakini polepole alianza kulizoea.

Kwa maelezo yake, alisema kuwa alipoteza meno yake katika ajali ya gari. "Nilikuwa katika mwendo mkali kwenye barabara kuu na huku nikisikiliza simu yangu ya mkononi. Nikaghafilika, badala ya kupunguza mwendo na kupinda kushoto, nilipinda kulia. Nilikutana uso kwa uso na lori lililokuwa na bidhaa mbalimbali. Ninakumbuka nilisikia mlio mkubwa. Baada ya hapo, sikufahamu tena kilichoendelea."

Mzee Nyange anasema alipozinduka alijikuta yupo kitandani katika hospitali ya Mnazimmoja ambako alilazwa kwa mwezi mzima. Pembeni walikuwa wamesimama wauguzi wawili na daktari mmoja. Wote hao walikuwa wakimpatia huduma. Muuguzi mmoja alikuwa anarekebisha chupa ya maji waliyomtundikia na mwengine alikuwa akimfuta damu kwenye majeraha aliyoyapata.

Katika ajali hiyo mzee Nyange aling'oka meno yote ya mbele, juu na chini na kuwa kibogoyo. Alipata maumivu makali ya mbavu na mwili wote kwa ujumla.

Mzee Nyange hivi sasa ni dereva makini sana. Amekuwa muhamasishaji mzuri wa usalama barabarani.

Maswali

a) Kwa nini mzee Nyange aliitwa kibogoyo?

b) Taja tahadhari mbili (2) ambazo mzee Nyange alipaswa kuchukua ili kuepuka ajali.

c) Mzee Nyange alikaa hospitali kwa muda gani?

d) Bainisha athari mbili (2) alizozipata mzee Nyange baada ya ajali.

e) Eleza namna tabia za mzee Nyange zilivyobadilika baada ya kupata ajali.

2. Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari katika habari uliyoisoma.

i. _____

- ii. _____

- iii. _____

- iv. _____

- v. _____

SEHEMU B: (Alama 40)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Taja aina za vivumishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Skuli yetu inapendeza.

ii. Wanafunzi wangapi wamefika mapema?

iii. Mtoto yule ana nidhamu sana.

iv. Mayai matano yamevunjika.

v. Miti enyewe imekauka yote.

4. Badilisha sentensi zifuatazo katika hali ya umoja.

Kwa mfano: Nazi zimefuliwa.

Nazi imefuliwa.

i. Watoto wanaogelea baharini.

ii. Wanafunzi wamefaulu vizuri mitihani yao.

iii. Walimu wetu wanasomesha kwa bidii.

iv. Sisi tunapenda kwenda skukuuni.

v. Mbuzi wamevunjika miguu.

5. a) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Eelfu tisa mia tatu na sabini na mbili.

ii. Laki tatu na elfu sabini na tano.

iii. Efu thelathini na nne mia tatu na kumi na mbili.

b) Andika sentensi zifuatazo kwa Kiingereza.

i. Baba yangu ni rubani.

ii. Tunacheza mpira wa miguu kila wiki.

6. a) Andika maelekezo matatu (3) ambayo mzazi anaweza kuyatoa kwa mtoto wake.

i. _____

ii. _____

iii. _____

b) Toa taarifa fupi ya tukio ambalo huwezi kulisahau katika maisha yako.

Nambari ya Mtahiniwa _____

8. a) Kamilisha methali zifuatazo.

- i. _____ chema huvishwa pete.
- ii. _____ si mkulima.
- iii. Njia ya mwongo _____

b) Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kuandika jawabu kwenye mabano.

- i. Ukoo wetu hauishiwi na safari. (_____)
- ii. Babu yangu ni tajiri wa rangi. (_____)

SEHEMU D: (Alama 20)

UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Andika barua kwa kaka yako anayeishi Tanga na umueleze jinsi ulivyojitayarisha na mtihamu wako wa mwisho wa mwaka na matarajio yako yatakapotoka matokeo.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal blue or grey ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There is no handwriting or other markings on the paper.

Nambari ya Mtahiniwa _____

-
- This image shows a single sheet of white paper with horizontal blue or grey ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There is no handwriting or other markings on the paper.

=====